

LEARNING BY EAR 2009

Economics – 4th episode

SUCCEEDING IN THE BUSINESS WORLD

Series: “THE STORY OF TWO YOUNG PEOPLE, WHOSE
SUCCESS STEMS FROM THEIR POCKET MONEY”

Author: Frédéric GAKPARA

Editors: Yann Durand and Sandrine Blanchard

Translator: Anne Thomas

Kiswaheli Eric Ponda

FOURTH EPISODE: "The harsh reality of the business world."

Characters: **John** (*17-year-old boy, twin.*)

Jane (*John's twin sister*)

Dad (*Twin's 46-year-old father.*)

Granma (*Twin's 67-year-old grandmother.*)

Ayaba (*20-year-old woman, Granma's domestic help.*)

Customer (*30-year-old woman.*)

Intro

NARRATOR: Karibu tena msikilizaji tunapoungana katika makala haya ya Learning By Ear, ikiwa ni mfululizo wa vipindi vinavyotayarishwa na Deutche Welle. Bado tunazungumzia suala la Uchumi. Na Hadithi hii inawangazia Vijana wawili mapacha ambao kwa juhudi zao za kuweka akiba sehemu ya pesa zao za matumizi, wamefanikiwa kuanzisha biashara yao. Kipindi cha leo tutaangalia **"Panda shuka katika ulimwengu wa Biashara,"**.

Mapacha hawa John na Jane sasa wanakumbwa na changamoto nyingi katika biashara yao, kufuatia mavuno duni hali inayosababisha kupanda kwa bei za mazao ya kilimo. Bei za Njugu ambazo ndio biashara yao pia zimepanda maradufu. Na wanalazimika kuvunja ahadi walizotoa za kuwasilisha bidhaa hiyo kwa wateja wao wa kudumu. Wanabiashara hawa chipukizi wanawasi kuhusu hali hiyo wanapojiandaa kwa mtihani wao wa mwisho hivi karibuni.

Scene 1, AT HOME, IN THE LIVING ROOM

JOHN AND JANE

ATMO: *Storm. The cat meows in fear. Television in the background, throughout the whole scene until line 20 of scene 2.*

- Jane:** Mvua imenza tena kunyesha! Baada ya msimu wake kumaliza!
- John:** Imesubiri hadi mazao yote yamekauka....!, hii ni hasara kubwa.!

3. **Jane:** Hatuwezi kutabiri chochote kwa kweli. Hakuna mtu ambaye yu-salama .Magazeti yanaandika kuhusu hali mbaya, majanga hasa,mafuriko kwa watu wasiohitaji mvua,ukame kwa watu wanaohitaji mvua, mitetemeko ya ardhi,.. moto kuteketeza misitu na kadhalika.....
4. **John:** Kila kitu kimepanda sokoni na bei bado zinazidi kupanda tu kila siku. Kweli sijakwambia kilichotokea siku ile? (*imitating a regional accent*) "*Wee rafiki yangu, usituongezee dhiki. Kuna watu wameshindwa kugharamia chakula mara tatu kwa siku na wewe uko hapa kuuza Njugu zako*" Niliudhika lakini kwa upande mwengine nikashikwa na moyo wa huruma!
5. **Jane:** Lakini ni kweli,... kwa muda wa miezi sita sasa bei za vyakula zimepanda maradufu. Mikahawa ambayo haijafungwa nayo imekataa kununua njugu zetu na sasa biashara yetu imekwama, hatujui tumuuzie nani.
6. **John:** (*To the cat, whistling.*)
MyaumyauPf* ! Pf* ! Pf* ! Njoo hapa Ketty. Ameogopa... (*To Jane*) Na sasa

nimeelewa kwani nini ulikuwa na wasi wasi wakati tukifungua akaunti ya benki siku ile.

7. **Jane:** Najua Kaka huwezi kunibwaga.
8. **John:** Wewe kila wakati unafikiria kuhusu suala hili. Sasa unapasa kutafuta njia za kujitoka kutoka balaa hili.
9. **Jane:** Kweli tutaweza kumudu hali hii ngumu ya uchumi huku tukiandamwa na kodi za kila aina,.. kama tunavyowasikia wenye mikahawa na maduka wakilalamika kila siku?
10. **John:** Katika muda wa miezi sita pekee mikahawa yote imefungwa!. Hebu fikiria!
11. **Jane:** Biashara yetu ilianza vizuri lakini imekuwa kama kimbunga tu.
12. **John:** Usikate tamaa Jane!, hiki ni kimbunga tu kitapita.Mambo yatabadilika baadaye.
13. **Jane:** Tuwe na matumaini lakini kati ya sasa na tutakapoanza likizo hapana shaka njugu zetu zitaoka.
14. **John:** Sasa tutafanya nini ?

15. ATMO: *The rain starts to fall. It sounds loudly on the tin roof. The cat continues to meow.*

NARRATOR: The twins can't stop complaining. Their father comes out of his room and goes and sits in the armchair opposite them.

Scene 2, AT HOME, IN THE LIVING ROOM

JOHN, JANE, DAD

16. Dad: Naweza kushiriki mazungumzo yenu ?

17. Jane: Tunajadiliana kuhusu taarifa za Televisheni Baba!.

18. Dad: Oh, kweli? ... Kwani siku hizi mumekua waandishi wa habari za televisheni?
(After a silent pause, he raises his voice.)
Kusema kweli mnanikasirisha na hiyo biashara yenu ya Njugu. Mnafikiri kuna kitivo cha msuala a Njugu katika chuo kikuu? Hivi karibuni mtihani wenu utaanza katika muda wa wiki nne zijazo, na hamujakuwa mukifanya vyema kwa kuzingatia matokeo yenu ya hivi karibuni. Nilidhani kuwa biashara hiyo ya njugu munaifanya wakati wa likizo kama sehemu ya mapumziko yenu? Lakini si usiku si mchana kazi biashara ya njugu. Ukipita huku ni Njugu, ukipita huko ni njugu,

hata kulala tunalala na njugu siku hizi? Hii inanikasirisha sana. Nyumba yangu ina nini lakini? Mumekosa nini wanangu? Hee...! mumekosa nini maishani? Kwani hamupati chakula, hamuvai au ni nini mnachokosa katika nyumbani hii?. Sasa Nataka kuwaona na vitabu vyenu mukisoma sasa hivi . Sitaki kusikia tena biashara ya Njugu katika nyumba hii!.... mmesikia?

19. Jane and John: Ndio Baba !

20. Dad: Funga hiyo televisheni haraka na muende chumbani kwenu haraka! Hata kama kesho ni Jumamosi!!
(*shouting*)

NARRATOR: John na Jane wanakwenda chumbani mwao kulala, lakini hawawezi kujizuia kuzungumzia suala kuhusu biashara yao.

Scene 3, IN THEIR BEDROOM

JOHN AND JANE

21. (*John and Jane are whispering*)

22. John: Kwa maoni yangu bado kunamatumaini!.
Watu hujifunza kutokana na makosa yao na

hivyo kuwawezesha kuwa imara kukabiliana na changamoto maishani.

- 23. Jane:** Nakubaliana nawe, lakini ni vipi tutaweza kuiokoa bishara yetu na tusife njaa wakati tunapo jifunza mambo yote haya?.
- 24. John:** Kwa wakati huu sijui lakini maoni yangu ni kwamba bora kununua njugu nyingi na kuzihifadhi wakati bei zitakaposhuka.
- 25. Jane:** Tutakuwa hatuja suluhisha chochote. Kwanza tutazihifadhi wapi ambapo hazitaharibika?
- 26. John:** Ohhhh... basi nipe suluhisho badala ya kuniuliza maswali mengi.! Tunaweza kuuza njugu wakati biashara ni nzuri tu, kama hatuwezi kupata mahali salama pa kuzihifadhi.
- 27. Jane:** Nimechanganyikia sasa John. Nipe muda wa kulifikiria suala hilo. (*Silence*) Au tumulize Bibi kesho kama anaweza kutupa ushauri kuhusu vipi tunaweza kuzihifadhi. Endapo tutavuruga mpangilio wetu wa biashara kuna tisho la kuwapoteza wateja.

- 28. John:** Ni kweli , na unajua kunawafanyi bishara wengine huko nje ambao wako tayari kuwanyakua wateja wetu.
- 29. Jane:** (*pensive*)
Tunaweza kufikiria uwezekano wa kusafirisha njugu zetu katika soko la Ulaya, lakini sijui tutaanzia wapi!
- 30. John:** (*enthusiastically*)
Hilo haliwezekani , Jane! Au tunaweza kumshauri Baba mdogo Sami amekuwa akiishi Zurich kwa muda sasa. Yeye anaweze kutupa ushauri.
- 31. Jane:** Pia kuna Fo Blam mjini Frankfurt. Ameishi huko kwa muda wa miaka 20 sasa
- 32. ATMO:** *The storm rages outside, there is silence in the room.*
- 33. John:** Unalala ?
- 34. Jane:** Hata bado sijalala!.
- 35. John:** Hata mimi siwezi kuu.....
(*Silent pause*)
Ninacho amini ni kwamba hatupasi kukata

tamaa, tumetumia pesa nyingi kuanzisha biashara hii.

- 36. Jane:** Kweli ,lakini kwanini tusibadilishe biashara yetu na kuanza kuuza bidhaa nyingine?
- 37. John:** Unasema nini wewe?
- 38. ATMO:** *The rain calms down a bit.*
- 39. Jane:** Nasema tuanze kuuza bidhaa nyingine badala ya njugu. Biashara ambayo tunaweza kuifanya kwa sasa hivi tunaposubiri msimu wa Njugu. Unanielewa.?
- 40. John:** *(He yawns)*
Ndio nakuelewa. Si wazo baya...Tayari nimeanza kufikiria ni biashara gani nyingine tunayoweza kufanya...
- 41. Jane:** *(Distantly)*
Katika biashara ni lazima utakumbana na panda shuka nyiingi...
- NARRATOR:** Matumaini yetu ni kwamba wawili hawa usiku huo walipata majibu ya maswali mengi waliyonayo. Asubuhi John na Jane

wanandamana kumtembelea bibi yao katika
kibanda chake cha biashara sokoni ...

Scene 4, AT THE STALL

JOHN, JANE, GRANMA, AYABA, CUSTOMER

- 42. ATMO:** *Loud market noise. Shouts, motorbikes ...*
- 43. Granma:** Ohhhh! Ndio sababu hamna furaha hivyo?
Mungekuwa na watoto au watu
wanaowategemea hapo ningeelewa lakini
Baba yenu anasema kweli. Wakati huu
mnapojiandaa kufanya mtihani mnapasa
kuzingatia masomo yenu .
- 44. Jane:** Sasa bibi si njugu zetu zitaoca!
- 45. Granma:** Hilo ndilo tatizo kubwa mtu anapofanya
bishara ya chakula. Kwa ufupi ni kwamba
kunapanda shuka nyingi katika biashara hii.
Lazima Mtu ajue njia ya kukabiliana na
mabadiliko ya mazingira katika biashara
hiyo. Labda muzikaange na kuzisaga ili
ziweze kutumiwa kwa mapishi?
- 46. John:** Huo ni ushauri mzuri, zikisagwa na
kuhifadhiwa kwenye chupa haziwezi
kuharibika?.

47. **Granma:** Haziwezi hata kidogo!
48. **John:** Unajulikana unga wa njugu karanga."
49. **Granma:** Pia mtu anaweza kutumia unga huo kutengeneza mchuzi. Ni rahisi na bora zaidi kuliko ule wa kawaida.
50. **Jane:** Hilo ni pendekezo zuri sana kwa hifadhi njugu tulizonazo ili tuepuke hasara.
51. **John:** Tutatafuta chupa nzuri na tuweke nembo ya kupendeza ili tueweze kuuza hata katika mataifa ya Ulaya, sivyo?
52. **Granma:** Tuna weza? Chochote chawezekana!
53. **Jane:** Usisahau bado tunafikiria biashara nyingine, tukisuburi msimu wa Njugu.
54. **Granma:** Pia hilo ni pendekezo zuri . Lakini tatizo ni kwamba kila kitu kimepanda bei sokoni. Watu siku hizi wananunua vitu muhimu tu kubania matumizi! Kodi inazidi kutumaliza. Nini unachoweza kuuza na uwe salama?. Hakuna! Hali iliyoko kwa hivi sasa si makosa yako.Ni tatizo la nchi nzima

- 55. John:** Kwa biashara hiyo tunaweza kununua kiasi kikubwa cha Njugu wakati msimu ni mzuri, na kusubiri hadi wakati wa ukame na kisha tukazisaga na kuuza unga katika soko la nje.
- 56. Customer:** Hili rinda ni pesa ngapi ?
- 57. Granma:** Karibu msichana karibu ndani! (*To Ayaba*)
Ayaba, msaidie mteja !
- 58. Jane:** Pia tunaweza kuuza njugu tunazotayarisha katika soko la mataifa ya Ulaya ikiwa watu huko watazipenda.
- 59. John:** Tulifikiri baba mdogo Sami na Fo wanaweza kutusaidia.
- 60. Ayaba:** (*To Granma*)
Bibi, huyu msichana anataka kununua rinda kwa faranga 3,000.
- 61. Granma:** (*To the Auntie*)
Oh, binti yangu, rinda linagharimu zaidi ya bei hiyo lakini kwa wewe chukua kwa bei hiyo mama. Wewe ni mteja wa kwanza hapa asubuhi ya leo.
- 62. Customer:** Asante sana Mama!

63. Granma: Kwaheri na uwe na siku njema! (*To John and Jane*) Nisikilizeni wajukuu zangu, munaweza kuwa na kipawa cha biashara lakini hamjakuwa wafanyi biashara. Bado nyinyi ni wanafunzi kwa hivyo ni bora mushauriwe mambo ya biashara na kuzingatia masomo yenu . Mtakuwa na wakati wa kutosha kuanzisha upya biashara yenu wakati wa likizo. Lakini kwa sasa munaweza kusaga njugu zenu na kuzihifadhi vizuri.Ni sawa?

64. John and Jane: Ndio bibi...

65. ATMO: *The sounds of the market fade out gradually...*

Outro

NARRATOR: Na hadi hapo tunafika misho wa makala haya ya nne kuhusu hadithi ya wanabiashara chipukizi, leo tukiwa tumezungumzia panda shuka wanazokumbana nazo katika uliwengu wa biashara ". John na Jane wameshikwa na wasi wasi kiasi cha kusahau masomo yao. Baba yao na Bibi yao pia wanalitilia mkazo suala la kuzingatia masomo yao

66. Closing soundtrack to be left running after the outro and brought up

NARRATOR: Yaonekana John na Jane wamevumbua njia nyingine ya kuendesha biashara yao. Na kama ilivyo kwa wafanyi biashara, changamoto ni jambo la kawaida. Je wataimudu hali hii na kujifunza kutoka kwa wafanyi biashara waliokomaa? Ili kujua mengi kuhusu masuala ya Uchumi na biashara, usikose kuungana nasi katika kipindi kijacho cha Noa Bongo. Pia ikipenda kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa dw-world.de/lb e
Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!

Music up

END